# Je, una maambukizi?

## Jua hatari yako ya sepsisi

## Je, Sepsisi ni nini?

Sepsis hutokea wakati mwili una mwitikio mkali kwa maambukizi. Sepsisi inaweza kuharibu sehemu nyingi za mwili kama vile moyo na mapafu na inaweza kusababisha kifo.

Sepsisi inahitaji matibabu ya dharura. Nafasi nzuri ya kupona kutokana sepsisi ni kutibu haraka.

## Dalili za sepsisi



Kupumua haraka au kukosa pumzi



Homa na baridi



Mapigo ya moyo ya haraka



Joto la chini la mwili



Kuhara



Utoaji wa mkojo kidogo au kutotoa kabisa



Kichefuchefu na kutapika



Uchovu mpya, kuchanganyikiwa, kusinzia au mabadiliko ya tabia



Maumivu au 'kuhisi mbaya zaidi kuliko hapo awali'

## Je, ni kitu gani ninahitaji kuangalia?

Maambukizi yoyote yanaweza kusababisha sepsisi. Maambukizi mengi hupona yenyewe, lakini unahitaji kujua ni kitu gani cha kufanya ikiwa dalili zitazidi kuwa mbaya.

Unapokuwa na sepsisi, unaweza kujisikia mgonjwa sana - mbaya zaidi kuliko hapo awali, kwa njia ambayo nitofautina ugojwa wa kawaida.

## Je, nifanye nini ikiwa nina wasiwasi?

Ikiwa unafikiri wewe au mpendwa wako anaweza kuwa na sepsisi, amini hisia zako, piga simu Zero Tatu (000) au nenda moja kwa moja hospitalini na umuulize daktari au nesi, 'Je, inaweza kuwa sepsisi?

**Ni sawa kuweza kurudi nyuma,** hata kama tayari umeenda kwa daktari.

**Kama huna uhakika, piga 13 HEALTH (13 43 25 84) wakati wowote kwa bure, ushauri wa siri kutoka kwa muuguzi aliyesajiliwa.**

DELIVERING FOR QUEENSLAND | Queensland Government

## Je, nani anaweza kupata sepsisi?

Sepsisi inaweza kuambukia mtu yeyote, hata vijana na wenye afya. Watu wengine wana uwezekano mkubwa wa kupata sepsisi kuliko wengine.
Unaweza kuwa katika hatari zaidi ikiwa:

- uko juu ya miaka 65 ya kuzaliwa
- kuwa na kinga dhaifu
- hivi karibuni alifanyiwa upasuaji
- ni wajawazito au wamejifungua
- ni Waaboriginal au Torres Strait Islander
- wanatibiwa saratani
- wana hali ngumu za kiafya
- wana majeraha ya kuungua, majeraha ya kukatwa na majeraha mengine
- wana COVID-19
- tayari walishawahi kuugua sepsisi
- ni mtoto mdogo kuliko mwaka1.

## Je, utajuaje muda wa kuuliza – 'Je inaweza kuwa sepsisi?'




Tazama video hii ya dakika 1 ili kujifunza zaidi kuhusu sepsisi.

## Jinsi ya kuzuia sepsisi?

Njia bora ya kuzuia sepsisi ni kuzuia maambukizi. Unaweza kufanya hivi kwa:

**kuzungumza na daktari wako** kama unaumwa

kukaa ukiwa **umefanya chanjo zote zinazotakiwa**

kusafisha **majeraha muda wote na kuyafunika** yanavyoendelea kupona

**kuosha mikono yako** marakwamara

**kujua** dakili za maambukizi na sepsisi.

SC26000479_V1.2 06/2026

**Shukrani**
Imetolewa kutoka Mtandao wa Sepsisi wa Australia, Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa, na Jumuiya ya Australasia ya Magonjwa ya Kuambukiza.

**Kanusho**
Karatasi hii ya habari inakusudiwa kwa madhumuni ya kielimu pekee na haikusudiwi kuchukua nafasi ya ushauri unaotolewa na wataalamu wa matibabu. Karatasi hii ya habari iko kwenye majaribio. Ili kutoa maoni tafadhali tuma barua pepel sepsis@health.qld.gov.au.